**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0756642864**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0763504832**

**Matron/Patron: 0712140102**

**Shule ya Sekondari MINZIRO**

**S.L.P 29, KYAKA-MISSENYI**

**Tarehe 08.04.2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .............**
**S.L.P ..................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MINZIRO HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI MKOA KAGERA, MWAKA 2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Minziro ipo umbali wa Kilometa 32 Mashariki mwa mji wa Bunazi. Usafiri wa basi kutoka mjini Bukoba unapatikana katika kituo cha

mabasi Bukoba, panda magari ya kwenda Mutukula ushukie Bunazi, nauli ni shilingi 8,000/= kwa pikipiki na shilingi 4,000/= kwa haisi kufika shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe....……...... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ......................

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruali 2 za rangi ya dark blue zenye mifuko miwili ya kawaida pembeni na mfuko mmoja nyuma wenye kifungo, mapana kwa chini (yaani miguuni) iwe na vipimo vya inchi 15-17 (zisiwe za mitumba).

ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu (tetroni). (yasiwe ya mitumba)

iii. Sare ya michezo ni bukta na T-shirt za njano kwa mchepuo wa PCB na nyekundu kwa mchepuo wa CBG na soksi pamoja na raba za michezo. Vitavaliwa wakati wa michezo uwanjani tu.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na soksi nyeusi jozi mbili au zaidi.

v. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali; usiwe na Bicross pana wala wenye maandishi au picha yoyote

vi. Sweta moja ya rangi ya kijivu kizito(Deep grey) yenye shingo duara nyuma na V yenye nembo ya shule

vii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali mbili nyeusi( vipimo vyake viwe sawa na vipimo vya kipengele(i) hapo juu.

viii. Tai moja dark blue yenye michirizi myeupe.

ix. Tisheti (T-shirt) za blue mbili zenye kola, ziwe nzito na ziwe na nembo ya shule.

ix Pair moja ya track suit rangi ya blue bahari

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Vifaa vya darasani( kalamu za wino, kalamu ya risasi, kifutio, rula, madaftari(countewr books) za kutosha na mkebe wa vifaa vya Hesabu( Mathematical set) bila kusahau kamusi ya kingereza

ii. **Ream (A4)** Moja na Ream ya karatasi za misitari (1) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika PCB na CBG
iv. Graph pad yenye karatasi hamsini
v. Kwanja 1, jembe moja, mfagio laini wa plastiki (soft broom) mmoja, mfagio mgumu wa plastiki(hard broom) mmoja, mfagio wa chelea mmoja na mopper/ flap moja (zinapatikana maeneo ya shule)
vi. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
vii. Scientific Calculator- non programmable (CASO fx-991MS)
viii. Stop watch (digital)
ix. Godoro moja la sponji size futi 2 na nusu kwa sita (21/2X6)
x. Kandambili, taulo,fulana mbili vyeupe(vest) boksa 2 au zaidi, sabuni za kufulia na kuogea, mafuta ya kujipaka, mswaki na dawa ya meno na toilets papers.
xi. Mashuka Jozi 2 pinki, blanket 1, foronya ya godoro 1 pinki, chandarua 1 (Chandarua ni muhimu sana)
xii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xiii. Jaketi jeusi(sio koti) kwa ajili ya kujikinga na mvua pia kujikinga na baridi kwa mgonjwa wa kifua na mwenye cheti cha daktari ambalo lazima livaliwe juu ya shati la shule.
xiv. Vitambaa vya mkononi( leso) viwili au zaidi.
xv. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xvi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
xvii. Aje na passport size nne(4) apige akiwa amevaa sahati jeupe kitambaa cha nyuma kiwe cha bluu.

### 2.3 Michango ya uendeshaji wa shule ni Tsh. 80,000/=

**Fedha zote ziwekwe katika akaunt namba** 32601100036 katika benk ya NMB yenye jina MINZIRO SEKONDARY SCHOOL RECURRENT ACOUNT

**Aje na bima ya afya**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya RaisTAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**ANGALIZO**

**Mwanafunzi atakayepoteza kifaa chochote cha shule kwa uzembe au makusudi mengine na akabainika atatakiwa kununua kifaa kingine cha aina hiyo hiyo ili kulipa upotevu huo.**

**KIAMBATISHO A**

Anwani ………………………………………
………………………………………………..
………………………………………………..
………………………………………………..
Tarehe ………………………………………..Mkuu wa Shule,

Mkuu wa shule,
Shule ya Sekondari Minziro,
S.L.P 29,
Kyaka- Missenyi.

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MINZIRO**

Mimi ……………………………………………………………………… *(Jina la mwanafunzi)* nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha TANO katka Shule ya Sekondari Minziro kuanzia mwaka …………………
*__Nakubali/ Sikubali__ nafasi hiyo. **Nimesoma na kuelewa Sheria na masharti ya kujiunga na shule hii yaliyoambatanishwa**. Hivyo ninaahidi kujifunza kadri ya uwezo wangu wote bila kupoteza muda au kufanya mzaha wowote kama Sheria zilivyo ainishwa. Nitatimiza wajibu wangu wote kwa muda na wakati uliopangwa. Pia ninaahidi kuwa nitatii sheria zote za shule**. Endapo nitashindwa kutii na kufuata sheria hizo hatua zinazostahili zichukuliwe dhidi yangu**. Natoa ahadi hizi mbele ya Mzazi/ Mlezi wangu, ambaye naye ametia sahihi yake kwenye kifungu kinachofuata hapa chini.

…………………  ……………………

***SAHIHI YA MWANAFUNZI*** ***TAREHE***

Mimi ………………………………………………………………. (Jina la *Mzazi/ Mlezi)
*Nakubali/ Sikubali mtoto wangu ajiunge na Shule ya Sekondari Minziro. Nimesoma na kuelewa sheria na masharti ya kujiunga na Shule hii. Hivyo nakubaliana na masharti na sheria hizi ambazo itambidi mwanangu azifuate kama alivyoahidi mbele yangu. Nipo tayari kulipa Ada na michango yote. Nitashirikiana na uongozi wa shule pamoja na jumuiya nzima ya shule katika kutoa malezi bora kwa mwanangu kulingana na sheria za shule na matakwa ya Taifa kwa ujumla.
Taarifa na mawasiliano yote yahusuyo mwanangu yatumwe kwangu kwa kutumia anwani ifuatayo:

……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………
………………………… ………………………… Namba za simu : ……………………

Mabadiliko yoyote ya anwani yangu nitayatuma kwa Mkuu wa Shule kwa maandishi.
Sahihi ya **Mzazi/ Mlezi* ………………………………………………….
Tarehe ………………………………
***Futa isiyotakiwa**

## KIAMBATISHO B
## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ………………………………………………………………………………….

*(kama lilivyo kwenye Form Four SEL Form na Birth Certificate)*

1 .Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………...

2. Anwani ya nyumbani ……………………………………………………………………

3. Mahali unapoishi (Nyumbani kwenu): Wilaya ………………………Tarafa ……………
Kata …………………………….. Kijiji …………………………………………….......
4Anwani ya nyumbani ……………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
5. Dini ………………………………………………………………………………...
6. Kabila ……………………………………………………………………………………
7. Taifa *(Mtanzania/ si Mtanzania)* ……………………………………………………..
8. Jamaa katika familia*: (Watakaohusishwa katika malezi ya mwanafunzi akiwa hapa shuleni)*

i.Jina la Baba ……………………………………
Anwani …………………………………………… SIMU NA.1 ………………
Anaishi/ Haishi …………………………………… 2 …………
Kazi yake …………………………………………

| Picha ya Baba mzazi |
|---|

ii.Jina la Mama ………………………………………
Anwani …………………………………………… SIMU NA.1 ………………
Anaishi/ Haishi …………………………………… 2 …………
Kazi yake …………………………………………

| Picha ya Mama mzazi |
|---|

iii.Jina la Mlezi ………………………………………
Anwani ……………………………………………
…………………………………………………….. SIMU NA.1 ………………
Kazi yake …… …………………………………… 2 …………
Uhusiano wake na wewe ………………………….

| Picha ya Mlezi/ Ndg wa karibu |
|---|

iv. Jina la Mlezi ………………………………………
Anwani ……………………………………………
…………………………………………………….. SIMU NA.1 ………………
Kazi yake …… …………………………………… 2 …………
Uhusiano wake na wewe ………………………….

| Picha ya Mlezi/ Ndg wa karibu |
|---|

v. Idadi ya Kaka ………………………………………………………………………
vi. Idadi ya Dada ………………………………………………………………………
vii. Wewe ni wangapi katika familia ………………………………………………..

Mimi …………………………………… *(mwanafunzi)* nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza ni za kweli.

……………………………                                                  ………………
*Sahihi ya Mwanafunzi*                                                  *Tarehe*

Mimi ………………………………… *(Mzazi/ Mlezi)* wa mwanafunzi ……………………............................... nimehakikisha kuwa taarifa zilizojazwa hapo juu ni za kweli.

……………………………….
*Sahihi ya Mzazi/ Mlezi*
*Tarehe…………………..*

*Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa ……………………………………………….
Sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa …………………  Tarehe ………………
Simu Na.1 ………………………….. 2 ………………………… 3 …………………

KIAMBATISHO C
MISSENYI DISTRICT COUNCIL

Minziro secondary school,
P.O.Box 29,
Kyaka- Missenyi.
Date ………………….

To Medical Officer,
…………………………………….
……………………………………..
…………………………………….

…………………………………….

**Ref: …………………………………………………… (Name of student)**

Please examine the above named student as per Medical examination form below:

……………………………..

**HEADMASTER**

MEDICAL EXAMINATION FORM

**(To be completed by Government Medical Officer)**

Full Name ………………………………………………………………………………

Age ……………………. Height ……………… (cm) Weight ……………….. (Kg)

1. Blood count
2. Stool Examination …………………………………………………………………….
3. Urinary ……………………………………………………………………………..
4. STDs and other V.D …………………………………………………………………..
5. T.B. and Leprosy test …………………………………………………………………
6. Eye test ……………………………………………………………………………..
7. Ear test ……………………………………………………………………………..
8. Chest ………………………………………………………………………………
9. Abdomen …………………………………………………………………………...
10. Spleen ………………………………………………………………………………

Any additional information:

E.g. Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases (eg. Sickle cell), in ability to eat certain foods etc.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

I have examined the above named student and I certify that he/ she is ***FIT/ NOT FIT*** to pursue Secondary Education.

……………………………………. ……………

*Signature and Official Stamp* *Date*

Station ………………………. Designation ………

**KIAMBATISHO D**

**ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI**

Mzazi unashauriwa kumnunulia mtoto wako vitabu kwa kila somo analokuja kusoma kama ilivyoainishwa hapa chini.

BIOLOGY

i. Biology Science by DJ Tylot
ii. Understanding Biology for Advanced level by Grenn & Susan
iii. Advanced Biology Principles and Application by C.J.elegga and DG Mackean

CHEMISTRY

i. Inorganic chemistry by TIE (Part 1 & 2)
ii. Physical chemistry Vol. I and II
iii Physical chemistry by Chand
iv. Organic chemistry by TIE

PHYSICS

i. Advanced Physics 7th Edition by Nelcon & Parker
ii. A level Physics by Rodgers Mancaster
iii .Essential Principles of Physics 2nd Edition by Whelang Hagson

GEOGRAPHY

i. Fundamental Geography By Josephat Mwita A.M
ii .Physical Geography By Monk House
iii .Practical Geography For Africa By John Richard

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na kitabu cha somo la General Studies (Understanding Advanced General Studies by J. Bigirwamungu & Sospeter) na somo la Basic Applied Mathematics (Basic Applied Mathematics by MAT).

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ........................**

**Jina la Mkuu wa Shule .........................**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule ...................**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0673967489/ 0756642864/ 0782168662**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0763504832/0675997388**
- **Mwandamizi Taaluma 0754694112**
- **Mwandamizi Malezi 0757141124**